

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Telagrams: "REGCOM COAST"

Tel. No. 023-2402287/2402066

Fax No. 023-2402358/2402151

E- Mail: [ras@pwani.go.tz](mailto:ras@pwani.go.tz)

[ras.pwani@pmoralg.go.tz](mailto:ras.pwani@pmoralg.go.tz)



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

Mkoa wa Pwani,

S. L. P 30080,

**KIBAHA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo ametoa agizo la kuwataka Madereva wa Pikipiki maarufu kama Bodaboda Wilayani Rufiji kusitisha huduma za kubeba abiria ifikapo **saa 12.00 jioni** kuanzia **Tarehe 29 Machi, 2017.**


Agizo hilo limekuja kufuatia mtiririko wa matukio yanayoendelea ya mauaji kwa Wenyeviti wa Chama na Serikali ngazi ya vijiji, huku wahusika wa mauaji hayo wakionekana kutumia usafiri wa pikipiki.

***"Madereva wa Pikipiki (Bodaboda) Wilayani Rufiji mnaifahamishwa kwamba kuanzia leo tarehe 29 Machi, 2017 usafiri wa pikipiki utasitishwa ifikapo saa 12.00 jioni. Huduma hiyo itafanyika kuanzia saa 12 Asubuhi mpaka saa 12 jioni. Lengo letu ni kuweza kuwabaini wahalifu wa mauaji haya. Hivyo naomba Wananchi wa Rufiji muwe wavumilivu katika kipindi hiki ambacho agizo hili litakuwa linatekelezwa".***

Aidha, Mkuu wa Mkoa amesisitiza kuwa, kwa yeyote ambaye ataenda kinyume na tamko hili atakamatwa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa, pia amewataka Wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili kuweza kuwabaini wahalifu hao.

Agizo hili litaendelea kuwapo Rufiji hadi hapo mtakapoelezwa vingine.

Imetolewa na:

  
Afisa Habari

**OFISI YA MKUU WA MKOA PWANI**

**29 Machi 2017**